



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA

Barua zote zitumwe kwa:

Simu: +255 28 2224013

Mkurugenzi Mtendaji (W),
S. L. P 131,

Faksi: +255 28 2224168

Muleba, Kagera.

Barua Pepe: ded@mulebadc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja

Kumb. Na. KGR/ML/HW/I.109/02

TAREHE 03/03/2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA
UKUSANYAJI WA TAARIFA ZA ANWANI YA
MAKAZI NA POSTKODI HALMASHAUARI
YA WILAYA YA MULEBA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba anapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa kuna nafasi za ajira ya muda kwa ajili ya kukusanya taarifa za anwani za makazi katika Vitongoji vyote vilivyoko Halmashauri ya Wilaya ya Muleba. Kwa mantiki hiyo zingatia yafuatayo:-

A. SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe Raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-35
- ii. Awe mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba
- iii. Awe na Elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea
- iv. Awe anamiliki simu janja (smart phone) inayotumia mfumo wa uendeshaji wa android (android OS) yenye uwezo wa kukaa na chaji siku nzima (24hrs)
- v. Awe na barua pepe (email address) na nywila (password) inayofanya kazi.
- vi. Awe na uwezo wa kusoma kutafsiri ramani za kitongoji
- vii. Awe ni mkazi wa Kijiji/Kitongoji husika
- viii. Awe tayari kufanya kazi katika Kata yoyote ndani ya Halmashauri ya Muleba

B. KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kujaza na kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- ii. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- iii. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia program tumizi ya mfumo wa anwani za makazi.
- iv. Kutumia data kwenye mfumo wa anwani za makazi
- v. Muda wa kazi utazingatia mkataba wa kazi

C. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA

- i. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
- ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- iii. Picha mbili za passport size
- iv. Barua ya maombi iliyopitishwa na Mtendaji wa Kijiji na wale walioko Mamlaka ya Mji mdogo barua ipitie kwa Mtendaji wa Kata.


D. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu inayopatikana muda wote pamoja na barua pepe (E-mail) inayofanya kazi na kuwasilishwa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba kwa anwani ifuatavyo;

MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA MULEBA
S.L.P 131,
MULEBA.

E. MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 09/03/2022 saa 9:30 Alasiri.


Charles L.M Ntaki,

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W),

